

Pambazuko

Toleo Namba 0040

Jumatatu Juni 5-11, 2023

Mpango wa Marekani washtua

Habari Zaidi Uk. 11

**CHALAMILA
ASIMCHULIE
RAIS SAMIA
Uk. 13**



**Akiba fedha
za kigeni
yaporomoka**

Uk. 9

Tahariri: Kwetu Yanga ndiyo bingwa

Uk. 2

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Kwetu Yanga ndiyo bingwa

MATUMAINI ya Tanzania kuandika historia ya kuwa na timu ya mpira wa miguu bingwa wa Afrika, yalifika kikomo Jumamosi – Juni 3, huko Algers, Algeria.

Ukomo huo ulitokana na mwakilishi wa Tanzania, Timu ya Yanga, kushindwa kuchukua Kombe la Soka la Shirikisho Afrika (CAF), kwa kanuni ya bao la ugenini lililofungwa na Timu ya USM Alger katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam, wiki moja iliyopita. Yanga ililala nyumbani kwa mabao 2-1.

Pamoja na Yanga kuwafunga wapinzani wao, wakiwa nyumbani kwao, bado timu hiyo ya Tanzania ikakosa ubingwa wa Afrika. Yanga ilishinda kwa bao 1-0 lililopachikwa wavuni na Djuma Shaban kwa njia ya penalti katika dakika ya saba tu ya mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Julai 5, 1962.

Timu ya Yanga ikaibuka kuwa mshindi wa pili na kuifanya kupokea Shilingi bilioni 2.3. Mshindi ameweka kibindoni Shilingi bilioni 4.7.

Hakika Yanga, pamoja na kukosa kombe hilo, mchezo wake wa marudiano, ilionyesha kiwango kikubwa mno cha kusakata kabumbu tofauti na mchezo wake wa kwanza uliochezwa Dar es Salaam.

Kiwango cha mpira kwa kila mchezaji kilionekana dhahiri kwamba Yanga walikuwa vitani na walienda kwa ajili ya ushindi, bila hofu kwamba wako ugenini, tena nchi ambayo ina mazingira na hali ya hewa tofauti kabisa

na waliyoizoea wachezaji wake. Baridi dhidi ya joto la Dar es Salaam.

Mpira walioupiga Yanga uliwatia hofu wapinzani wao, ambao walianza vitimbwi vya kucheza mchezo wa “kutegea na kulazimisha adhabu,” ingawa mwamuzi aliwashtukia mapema.

Hata kabla ya kuingia uwanja; usiku wa manane kuamkia siku ya mchezo, mashabiki wa Alger, ama kwa kutumwa ama kujituma, walifanya vituko kadha wa kadha kwa Yanga, ikiwamo kuzonga usingizi wa wachezaji walipokuwa hotelini. Walianza kurusha fataki ili kuwavuruga na kuwajengea woga wachezaji wa Yanga.

Wachezaji wa Yanga walipoingia uwanjani, walionekana kutokuwa na woga, walianza mchezo wao kwa kujiamini na kwa dakika za nyingi za mchezo huo, Yanga walisomeka kuongoza kiwango cha umiliki, hali ambayo ingewasaidia kuandika mabao, hata hivyo bahati haikuwa yao.

Pia ukiacha wachezaji wa ndani, kipa wa Yanga, Djigui Diarra alionyesha umahiri wake kwa kudaka mkwaju wa penalti uliopigwa na nahodha wa USM Alger, Zineddine Belaid.

Ni kutokana na kiwango hicho, na kupata bao dhidi ya wapinzaji wao – wakiwa nyumbani, sisi katika gazeti la Pambazuko tunabaki na imani kwamba Yanga ndiyo mabingwa wa michuano hiyo yenye hadhi kubwa Afrika, ukiacha Kombe la Mabingwa Afrika.

Tunaipongeza sana Yanga na kuipa shime kwamba wameweza.

SALUTI KWAKO MKUU...



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe akipokea saluti kutoka kwa askari baada ya kutua Mjini Igunga, Tabora - Mei 29, kuanza ziara ya Operesheni 255 ambayo inahimiza kuwepo kwa katiba mpya (Picha kutoka tovuti ya Chadema).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



"Maneno haya yanatusaidia kwa sababu yanatufundisha ukomavu, yanatufundisha kuwa na subra, yanatufundisha kuwa na uvumilivu na yanatujenga kuwa viongozi bora zaidi. Sisi tumesema waendeleo kwa sababu yanatusaidi. Sisi kisasi chetu ni matokeo -" Waziri wa Nishati, January Makamba akisungumsa bungeni wakati wa kuhitimisha bajeti ya wizara yake (2023/24) juu ya namna anavyosemwa mitandaoni.

Tafakuri

Tusikumbatie siasa za shari

Na Mwandishi MAALUM

MATUNDA ya amani ya Tanzania na watu wake hayakuota tu kama nyasi nyikani.

Miche yake ilipandwa, ikatunza, ikamea na hatimaye kuonekana na kuleta faida ya watu kupendana, kuaminiana na kuthaminiana kwa michango yao katika ujenzi wa taifa.

Amani hiyo ilitawala kwa miaka mingi; kuanzia uongozi wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, akifuatiwa na marais waliomrithi kwa vipindi tofauti; Alhaj Ali Hassan Mwinyi, Benjamin Mkapa, Jakaya Kikwete, John Magufuli na sasa Samia Suluhu Hassan.

Hata hivyo, lazima kuweka historia sawa, kwamba amani hiyo iliyotunzwa miaka nenda-rudi, ilivurugwa mno katika utawala wa Rais Magufuli, na Tanzania – kwa mara kwanza ilijenga matabaka ya imani za vyama, kiasi cha kupoteza amani.

Kwamba katika kipindi cha miaka zaidi ya sita ya utawala wa Rais Magufuli, wananchi wasiokuwa wafuasi wa chama tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM) walionekana maadui na kwamba hawana uzalendo.

Hali hii inayoweza kujenga tafsiri kuwa ni ushamba, ikabebwa na hata baadhi ya idara za usalama na kuanza kuonea na kutesa wasiokuwa waumini wa CCM. Ni katika kipindi hicho tulishuhudia wapinzani na waandishi wa habari wakiteswa, kuonewa na hata kupotezwa.

Ni kwenye kipindi hicho, baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa na waandishi, walikamatwa, kuharibiwa biashara zao, kupigwa risasi na wengine kubambikwa kesi za ugaidi, ubakaji na makosa mengine makubwa.

Shukurani kuu kwa Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye baada ya kuingia madarakani, aliamua kurejesha Tanzania katika misingi yake ya kuwa nchi yenye amani na watu wake kupendana na



Mwl. Julius Kambarage Nyerere

kushirikiana, bila kuweka imani na mapenzi kwa vyama vya siasa.

Hata hivyo, kumeanza kujitokeza chuki na minyukano ya baadhi ya wananchi, kisa kushabikia ama kuwa wafuasi wa vyama tofauti vya siasa. Jambo hili ni baya na linapaswa kukemewa kungali mapema.

Tumeathirika kiasi kwamba tunadhani siasa ni shari, na shari ni siasa. Ila hatupimi nguvu yetu na udhaifu wetu wakati wa shari.

Hata hivyo, tabia ya shari, chuki, hasira na visasi iliyojengwa kwa miaka sita mfululizo, haiwezi kuondoka ghafla tu, eti kwa vile kuna watu wanazungumza jinsi ya kuridhiana kitaifa.

Jambo lolote linalohusu tabia ya akili ya mtu, na linalotegema tabia hiyo, huhitaji muda kuibadili akili hiyo na mazoea yake.

Lakini tusiache mchakato ambao ndiyo njia ya kusahihisha mambo haya na kutuondoa katika siasa za hovyoo.

Siasa za ushari siyo nzuri. Hazitufikishi popote. Tuziepuke ili tuweze kusonga mbele kwa pamoja na kujenga Tanzania yetu.

Tuonyeshe upevu ili kukomesha siasa hizo, lakini kunahitajika kwanza kutuliza akili na kuongoza moyo.

Prof. Tibaijuka alilia uraia pacha

Na Tryruckia MFINANGA

WAZIRI wa zamani wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Prof. Anna Tibaijuka, ameeleza kukwerwa na namna Tanzania inavyokataa wananchi wake kuwa na uraia pacha.

Prof. Tibaijuka, ambaye ni mboenzi katika ustawi wa makazi na mazingira na siasa uchumi, amesema haoni kuwepo kwa sababu zozote za msingi za kukataa uraia pacha, badala yake ni kukwamisha maendeleo ya haraka kwa nchi na watu wake.

Amesema sababu kubwa ya Tanzania kukataa uraia pacha, wakati huo ikiwa Tanganyika, chini ya uongozi wa Rais Mwalimu Julius Nyerere, hazipo tena na kwamba dunia imebadilika mno kwa sasa ikilinganishwa na miaka mingi iliyopita.

Msomu huyo aliyewahi kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa (UN-Habitat), amesema miaka mingi iliyopita, mara baada ya uhuru, ilibainika kuwa Waasia na Waingereza wengi walikuwa wakimiliki mashamba na ardhi kubwa, hivyo kuwepo hofu kwamba endapo wageni wataamiliki maeneo makubwa, upo uwezekano wa wengine, hasa wazawa kukosa kabisa mahali pa kuishi na kuendeleza shughuli zao za kilimo na ufugaji.

“Wakati tunapata uhuru wageni walikuwa na nguvu sana kiuchumi, kisiasa na kitaalamu na hawa walimiliki ardhi kubwa. Wengine viwanda vikubwa hasa Waasia, huku wakiwa na uraia wa Uingereza, ikaonekana wakipewa uraia huku nako, watajiongezea maeneo zaidi, hivyo kuwanyima wengine – wasiokuwa na uwezo, fursa za kumiliki maeneo. Ndiyo ikawekwa marufuku,” anaongeza.

Amesema kuwa Mwalimu Nyerere aliamua kwamba wageni hao wasifukuzwe, lakini wachague kati ya Tanzania na huko walikutoka na wengi walichagua kuendelea kuwa raia wa Uingereza na Canada.

Prof. Tibaijuka anasema kutokana na



Prof. Tibaijuka. Picha imepigwa na Getty Images

kuwanyika fursa hiyo Watanzania, imefika wakati inaonekana Tanzania inanyanyasa watoto waliozaliwa nchini ambao sasa wako nje “wakitafuta maisha.”

Tayari Serikali ya Tanzania imeanza mchakato wa kutoa Hadhi Maalum kwa wananchi wake wanaoishi nje ya nchi hiyo ya Afrika Mashariki.

Serikali hiyo imeeleza kwamba uraia pacha kwa sasa haiwezekani, kwani hauna faida zozote kwa nchi na kwamba inapunguza uzalendo.

Msimamo wa Prof. Tibaijuka unaungana na idadi kubwa Watanzania ambao wamekuwa “wakipigania” kuwepo kwa uraia pacha kwa muda mrefu, huku serikali ikipinga.

Mwakilishi wa kundi la Watanzania waishio nje ya nchi, Liberatus Mwang’ombe wiki iliyopita alisema msimamo wa serikali kuhusu pingamizi la uraia pacha halitakuwa na manufaa kwa nchi.

Amesema hakuna sababu za msingi za Tanzania kukataa uwepo wa uraia pacha, badala yake ni kukwamisha maendeleo zaidi.

“Hadhi Maalum ni risiti ya kuukana uraia wa Tanzania, hata ukienda mahakamani itabidi watumie kielelezo hicho, yeyote atakayechukua hadhi maalumu atakuwa amechukua risiti ya kuukana uraia pacha,” amesema Mwang’ombe.

Habari

‘Serikali inaiua ATCL’

**Na Mwandishi WETU,
Dodoma**

HATUA ya serikali kuilazimisha Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) kukodi ndege kutoka Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA), ni moja ya sababu za kampuni hiyo kuendelea kupata hasara.

Akirejea ripoti ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka ulioishia Juni 2022, Mbunge Ester Matiko amesema ATCL imepata hasara ya Sh. bilioni 37

Mbunge huyo wakati akichangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka 2023/24, alitanabaisha kuwa katika kipindi cha mwaka huohuo, ATCL lililazimika kulipa kiasi cha Sh. bilioni 87 kwa TGFA kama malipo ya kukodi ndege.

“Hii ina maana kuwa kama serikali ingekuwa imeiwzesha ATCL kumiliki ndege hizi, basi mwaka huo ingepata faida ya Sh50 bilioni kwa sababu isingelazimika kutumia Sh. bilioni 37 kama malipo ya kukodi ndege,” alisema Matiko.

Mbunge huyo alishangaa ni kwa nini serikali inaendelea na utaratibu huo wa kuitaka ATCL ikodi ndege wakati taasisi hizo zote mbili, ATCL na TGFA, ni taasisi za serikali.

“Y a a n i kinachoonekana hapa ni serikali kujikodisha ndege yenyewe h a l a f u inajisababishia hasara yenyewe,” alisema Matiko.

Mbunge huyo alisema sababu

zilizotolewa awali kuwa ukodishaji ndege unafanyika ili kuondoa uwezekano wa ndege hizo kukamatwa na wadeni wa nje ya nchi kwa serikali haina maana kwa sababu hata ATCL imeshindwa kurusha ndege hizo kwenda kwenye baadhi ya maeneo kwa kuogopa jambo hilo.

Mbunge huyo alisema jambo hilo nalo linaisababisha ATCL hasara kubwa kwani haiwezi kuzitumia ipasavyo ndege hizo ilizolazimishwa kuzikodi.

“Hivi sasa ATCL haiweza kurusha ndege kwenda hata Afrika Kusini. Haiwezi kwenda Afrika magharibi au Marekani na hivyo kulisababisha shirika hasara kwa sababu ya ufinyu wa njia za kufanya biashara,” alisema.

Alisema inashangaza kuwa wakati hali ikiwa hivyo, bado serikali imeendelea kununua ndege nyingine kadhaa.

“Sasa hizo ndege nyingine mkizileta zitaruka kwenda wapi? Ni Dhahiri kuwa iwapo hayo madeni hayatalipwa, basi ndege hizi hazitakuwa na maana yoyote kwa sababu nazo hazitaruka kwenda

Inaendelea Uk. 7



Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan akiwa amekaa kwenye chumba cha marubani ya ndege mpya ya Misigo aina ya Boeing 767-300F ya Shirika la Ndege la Tanzania ATCL mara baada ya kuzindua katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam Jumamosi iliyopita - Juni 3. (Picha na Ikulu).

'Serikali inaiua ATCL'

Inatoka Uk. 6

kwenye masoko yenye faida,” alibainisha Matiko.

Katika hotuba ya bajeti aliyowasilisha, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema serikali inatarajia kupokea ndege nyingine nne. Hii ni baada ya kuwa na ndege 11, nyingi zikiwa zimenunuliwa chini ya uongozi wa serikali ya awamu ya tano.

Tayari ndege kubwa ya mizigo aina ya Boeing 767-300F, imewasili nchini wiki iliyopita.

Baadaye mwakani – 2024, serikali inatarajia kupokea ndege nyingine mbili na moja itapokelewa mwaka 2025.

Tayari pia Mkurugenzi Mkuu wa ATCL, Ladislaus Matindi amemuomba Rais Samia Suluhu Hassan kuridhia serikali kununulia ndege nyingine ya mizigo kwa kampuni yake ili kuweza “kuleta faida haraka.”

Akijibu hoja ya Matiko kuhusu ATCL kukodi ndege kutoka TGFA, Prof. Mbarawa alisema serikali ilishaliona jambo hilo na ili kulipatia ufumbuzi, Rais Samia Suluhu Hassan ameunda timu ya wataalamu ambao wanaliangalia suala hilo kwa undani.

“Timu hii inatarajiwa kutoa ripoti yake hivi karibuni na itaato mapendekezo ya nini kifanyike katika suala hilo,” alisema Prof. Mbarawa.

ATCL ni mwendo wa hasara

Pamoja na hoja hiyo ya Matiko, CAG katika ripoti yake anabainisha pia kuwa upungufu katika mkataba huo wa ukodishaji ndege ni jambo linalosababisha ATCL kulipa gharama mara mbili.

Akifafanua, CAG anabainisha kuwa ATCL ilitumia gharama za ziada za Sh. bilioni 19.11 ili kulipa Wakala wa Ndege za Serikali Tanzania kutotekeleza majukumu ya kimkataba.

Ndani ya mwaka 2021/22 ATCL ilikodi ndege 11 kutoka TGFA, hivyo kutozwa gharama za matengenezo za dola za Marekani 496 kwa saa moja kwa utendaji

kazi wa injini na dola za Marekani 360 kwa maisha ya injini ya mzunguko wa ndege, na kwa mwaka 2021/22 zilifikia shilingi bilioni 25.39 (2020/21 shilingi bilioni 18.56).

CAG anasema kiasi hicho ni kwa ajili ya matengenezo ya ndege zinapoharibika lakini jambo la kushangaza ni kuwa ATCL ililipa tena gharama za matengenezo ya ndege hizo hizo.

“Katika mapitio yangu ya gharama za uendeshaji, nilibaini kuwa, Kampuni ya Ndege Tanzania iliingia gharama ya shilingi bilioni 19.11 kwa ajili ya matengenezo ya ndege katika mwaka huo, ambayo ni sehemu ya akiba ya matengenezo chini ya mkataba wa Wakala wa Ndege wa Serikali ya Tanzania,” anabainisha CAG.

“Ni maoni yangu kuwa gharama hizi zilizoingiwa mara mbili zimesababishia kuongezeka kwa hasara kwa kampuni hii. Kwa kuwa, ulipaji mara mbili wa gharama ambazo ni shilingi bilioni 19.11 kwa watoa huduma na shilingi bilioni 25.39 kwa Wakala wa Ndege wa Serikali ya Tanzania, hasara iliyotokea mwaka huu ingeweza kupungua kutoka shilingi bilioni 35.24 mpaka shilingi bilioni 9.85,” anaongeza CAG.

CAG alitaka serikali kupitia kuharakisha mchakato wa kupitia makubaliano kati ya ATCL na TGFA ili kuhakikisha kasoro kama hizo zinarekebishwa.

Mbali na hilo, ripoti hiyo ya CAG kwa mwaka unaoishia Juni 2022 inaonyesha kuwa ATCL imekuwa ikipata hasara kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo.

“Pamoja na serikali kutoa ruzuku ya shilingi bilioni 30.63 kwa mwaka wa fedha 2021/22, kampuni bado iliripoti hasara ya shilingi bilioni 35.23. Serikali isingetoa ruzuku hiyo, kampuni ingepata hasara ya shilingi bilioni 65.86. Hii inaonesha changamoto ambazo Kampuni ya Ndege Tanzania inakabiliana nazo katika soko kwa sasa,” inasomeka sehemu ya ripoti hiyo.

Habari

Mafanikio PSSSF yawavuta Waganda

Na Malkia G'WANDU

MAFANIKIO makubwa ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) yamekuwa ya mfano kiasi cha kugeuka darasa la kujifunza kwa baadhi ya nchi za Afrika na taasisi za kimataifa.

Ujio wa kujifunza mafanikio hayo unafuata kuwepo kwa taarifa za kupunguza gharama za uendeshaji licha ya kuwa taasisi kubwa na yenye mtambuka wa majukumu baada ya kuunganishwa kwa mifuko minne na kuwa mmoja.

Mbali na kupunguza gharama, pia PSSSF inaelezwa kutoa huduma za kisasa zinazoendana na kasi ya kukua kwa teknolojia katika kuhudumia wateja wake; wastaafu pamoja na wanachama wengine.

PSSSF ilizaliwa Agosti Mosi, 2018 baada ya kuunganishwa kwa mifuko minne ya hifadhi za jamii; PSPF, PPF, GEFF NA LAPE.

Mfuko huo pia umekuwa ukisifika kwa kutengeneza mifumo rahisi na rafiki ya kukusanya michango kutoka kwa wanachama, hatua ambayo inahakikisha kila mwanachama anachangia kwa wakati.

Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, CPA. Hosea Kashimba anasema mfuko anaouongoza umekuwa na mafanikio makubwa ndani ya miaka mitano tangu kuanzishwa kwake, hatua ambayo imekuwa “gumzo” nchi nyingi hata kutamani kujifunza kutoka kwao.

Kutokana na mafanikio ya PSSSF, Serikali ya Uganda hivi karibuni ilituma ujumbe wa wabunge kufanya ziara ya mafunzo ya namna nzuri ya kujifunza uendeshaji wa huduma za hifadhi ya jamii kwa waajiriwa wa serikali.

Baada ya kumaliza ziara hiyo, mkuu wa msafara huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utumishi wa Umma, Catherine Musingwiire alishukuru uongozi wa PSSSF kwa kuwapata elimu na uzoefu



Kashimba

wa kina wa namna bora za uendeshaji wa mfuko huo.

Alisema tayari Uganda imo mbioni kuwa na mfuko wa namna hiyo na kwamba atahakikisha elimu waliyoipata PSSSF inaigwa katika uendeshaji wa mifumo ya kukusanya michango, uwekaji wa kumbukumbu za wanachama, huduma za kidijitali za wanachama pamoja na upande wa uwekezaji ili kuhakikisha uendeleu wa mfuko.

Mkuu huyo wa msafara alisema Uganda itajifunza mengi kutoka PSSSF na kwamba ana uhakika wa kupata mafanikio kwa kuwa wamejifunza kutoka kwa “waliofanikiwa.”

Katika ziara yao PSSSF, viongozi hao wa Uganda walijifunza mambo mengi ikiwamo mazingira wezeshi kuendana na mabadiliko ya kuendesha mifuko, ushirikishwaji wa utatu; serikali, vyama vya wafanyakazi na waajiri, huduma bora na matumizi ya teknolojia.

PSSSF hivi karibuni pia ilipokea ugeni kutoka Serikali ya Kenya, Benki ya Dunia na taasisi zingine za kimataifa kujifunza na kubadilishana uzoefu wa kuendesha mifuko.

Hivi karibuni, PSSSF ilipata tuzo na Taasisi ya Kimataifa ya Hifadhi ya Jamii (ISSA) kutokana na mafanikio yake.

Akiba fedha za kigeni yaporomoka

Na Mwandishi WETU

AKIBA ya fedha za kigeni katika hifadhi ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeshuka kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita, gazeti la Pambazuko limebaini.

Imebainika kuwa kiasi cha dola za Marekani milioni 569.1 ndicho kimepungua kwa mwaka wa fedha unaoshia karibuni; kuanzia Machi 2022 hadi Machi 2023.

Benki Kuu uhifadhi akiba ya taifa ya fedha za kigeni kwa mujibu wa vifungu vya 51 na 52 vya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, 2006.

Kiasi cha fedha za kigeni ambacho kinahifadhiwa na Benki Kuu kwa niaba ya serikali ni kwa lengo la kugharamia ununuzi wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi iwapo nchi itakumbwa na majanga yatakayoathiri mifumo yake ya kawaida ya ugazaji bidhaa.

Ripoti ya hali ya uchumi ya kila mwezi na ripoti ya hali ya uchumi kwa robo mwaka, ambazo zote zinatolewa na BoT, zimethibitisha kushuka kwa akiba hiyo katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita.

Hata hivyo, BoT imewataka wananchi kutokuwa na hofu na suala hilo kwa sababu akiba iliyopo inakidhi viwango vilivyowekwa na serikali na taasisi zingine za kimataifa.

Kwa mujibu wa BoT, kiasi kilichopo kwenye akiba hiyo hivi sasa kinatosheleza kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 4.5, ikiwa ni juu kidogo ya kipindi cha chini cha miezi minne kilichowekwa na serikali katika mipango yake ya uchumi.

“Kiasi cha akiba ya fedha za kigeni kimeshuka hadi kufikia dola milioni 5,012.5 mnamo mwezi Machi 2023 kutoka kiasi cha dola milioni 5,581.6 kilichorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022,” inasema ripoti ya hali ya uchumi kwa kila mwezi iliyotolewa hivi karibuni na BoT ikiakisi hali ya uchumi kwa mwezi Machi mwaka huu.

Hata hivyo, ripoti hiyo inaonyesha



Gavana wa BoT Emmanuel Tutuba

kuwa kiasi hicho kinatosha kuagiza huduma na bidhaa kwa kipindi cha miezi 4.5 kikiwa ni zaidi ya kiwango cha chini cha miezi minne kilichowekwa na nchi na kikilingana na kipindi cha miezi 4.5 kilichowekwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ambayo Tanzania ni mwanachama.

Kiwango hicho ni chini ya kile cha miezi sita au dola milioni 6,000 kilichowekwa na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), ambayo Tanzania ni mwanachama pia.

Ripoti hiyo inaonyesha pia kuwa katika muda mrefu kuanzia Septemba 2019 kiasi cha akiba ya fedha za kigeni kilikuwa ni pungufu kwa kulinganisha na thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje kwa mwezi.

Hali ilianza kutengemaa Machi mwaka jana, 2022 ambapo akiba ya fedha za kigeni ililingana na thamani ya bidhaa zilizoagizwa na nchi kwa mwezi na baada ya hapo kiwango cha akiba kikawa juu ya thamani za bidhaa zinazoagizwa kwa mwezi, hali iliyodumu kwa muda.

Aidha, kiwango cha akiba ya fedha za kigeni kwa kipindi kirefu kimekuwa chini ya kiwango kilichowekwa na SADC ambacho ni dola milioni 6,000 kinachoweza kuhimili kuagiza huduma na bidhaa kutoka nje kwa kipindi cha

Habari**Akiba fedha za kigeni yaporomoka***Inatoka Uk. 9*

miezi sita.

Pambazuko limebainisha kuwa ni katika kipindi cha kati ya Septemba 2021 na Machi 2022 pekee ndipo Tanzania iliweza kuvuka kiwango hicho kwa akiba yake ya fedha za kigeni kuwa zaidi ya dola milioni 6,000.

BoT inaeleza kuwa sekta ya biashara ya nje bado ipo katika hatari ya kuathiriwa zaidi na madhara ya majanga yaliyoikumba dunia katika miaka ya hivi karibuni likiwamo la janga la Covid-19, ambalo liliathiri bei za bidhaa duniani kwa kiasi kikubwa.

Kutokana na madhara hayo, BoT inabainisha kuwa kutokana na changamoto hizo nakisi ya biashara kwa nchi imeongezeka kwa kiwango kikubwa kutokana na ongezeko la bei ya bidhaa zinzoagizwa kutoka nje.

“Urari wa biashara ulirekodi nakisi ya dola milioni 874.2, ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 990 iliyorekodiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2022,” inabainisha BoT.

BoT inasema hali hii ni moja ya mambo yaliyochangia kuporomoka kwa akiba ya fedha za kigeni.

Deni la Taifa

Kwa upande mwingine, BoT inaonyesha kuongezeka kwa deni la taifa

na kufikia dola milioni 41,222.7 hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi mwaka huu. Hilo ni ongezeko la mwezi kwa kiasi cha dola milioni 354.3 kwa mujibu wa BoT.

Asilimia 71.8 ya deni hili ni deni la nje.

BoT inaeleza kuwa deni la nje liliongezeka kwa wastani wa dola milioni 541 mwa mwezi hadi kufikia dola milioni 29,605.1 mwishoni mwa mwezi Machi kutokana na kukopa zaidi.

BoT inasema kiasi cha dola milioni 57.0 zililipwa katika kipindi hicho zikijumuisha dola milioni 45.6 kama deni kuu na kiasi kilichosalia kikilipwa kama riba.

Kwa upande mwingine, deni la ndani lilipungua kwa Sh. bilioni 413.2 na kufikia Sh. bilioni 26,853.4 mwishoni mwa mwezi Machi mwaka huu.

Kupungua huko kulitokana na hatua ya serikali kulipa sehemu kubwa ya madeni hayo kulinganisha na kiwango cha hati fungani ambazo zilizuwa.

Kiasi kikubwa cha deni la ndani ni hati fungani za serikali ambazo zinafanya asilimia 79 ya deni lote.

Benki za biashara na mifuko ya hifadhi za jamii ndio wakopeshaji wakubwa kwa serikali huku madeni ya taasisi hizo kwa pamoja yakiwa ni zaidi ya asilimia 57 ya deni lote la ndani.



Mpango wa Marekani washtua

**Na Mwandishi WETU,
Dodoma**

SERIKALI ya Tanzania imetakiwa “kuamka haraka” na kuanza mchakato utakaowezesha kuimarishwa kwa mtandao wa unaunganisha nchi na Zambia pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Tahadhari hiyo imetolewa ikiwa ni njia ya Tanzania kukabiliana na ‘madhara’ yatakayotokana na uamuzi wa Marekani kugharamia uendelezaji wa reli kati ya Angola na DRC.

Mbunge wa Kilosa, Prof Palamagamba Kabudi, ameweka hadharani hadhari hiyo wakati akijadili hotuba ya bajeti ya wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka 2023/24.

Prof. Kabudi alionya kuwa kuimarishwa kwa reli hiyo inayojulikana kihistoria kama Korido la Lobengula au Reli ya Lobito, kunaweza kusababisha Bandari ya Dar es Salaam kupoteza sehemu kubwa ya biashara.

Lakini, alisema, iwapo serikali itaimarisha njia za reli zinazoungana na reli hiyo ya Lobito, upo uwezekano mkubwa wa kuongeza biashara kupitia Bandari ya Dar es salaam.

Akifafanua zaidi, Prof. Kabudi alisema kuwa iwapo Reli ya Lobito itaimarishwa wakati Tanzania haijaunganishwa katika reli hiyo, mizigo mingi kutoka Zambia na DRC itasafirishwa kupitia Bandari ya Lobito nchini DRC ambayo iko umbali mfupi kulinganisha na masafa kuelekea Bandari ya Dar es Salaam.

Kwa upande mwingine, Prof. Kabudi alisema kuwa iwapo njia ya reli kutoka Tanzania itaunganishwa na reli hiyo, upo uwezekano wa mizigo mingi, hasa kutoka nchi za Marekani Kaskazini na Kusini, kusafirishwa kupitia Bandari ya Dar es Salaam kuelekea Bara la Asia na Mashariki ya Mbali, kwani reli hiyo itafupisha safari ya kuzunguka Afrika Kusini au kupitia Mashariki ya Kati, eneo ambalo halina usalama wa uhakika.



Prof Kabudi

“Iwapo tutaimarisha reli mathalan ya Tazara ikaunganishwa na Reli ya Lobito, ina maana tutakuwa tumetengeneza kiunganishi kati ya Bahari ya Atlantiki upande wa magharibi na Bahari ya Hindi upande wa mashariki...

... Hii itarahisisha usafirishaji wa shehena hasa kutoka nchi za Marekani kuelekea Asia na Mashariki ya Mbali kwa sababu umbali utapungua sana kwa kutumia reli hiyo na Bandari ya Dar es Salaam,” alifafanua Prof Kabudi.

Kwa mujibu wa taarifa ya Ikulu ya Marekani, nchi hiyo inafikiria kutoa kiasi cha dola milioni 250 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa kufufua njia ya reli kati ya Angola na DRC inayojulikana kama Korido la Banguela.

Korido hilo linatengenezwa na reli kutoka mji mkuu wa Angola, Luanda, hadi katika mji wa pwani wa Lobito, katika Bahari ya Atlantiki kupitia Zambia.

Inaaminiwa kuwa ujenzi wa reli hiyo, ambayo umekuwa ukizungumzwa kwa muda mrefu, utaziwezesha nchi za Zambia, DRC na Angola kuitumia bandari hiyo ya Lobito kusafirisha mizigo yake kwa sababu ya ufupi wa safari kuifika bandari hiyo.

Hivi sasa, Bandari ya Dar es Salaam inategemea shehena kubwa ya mizigo

Habari**Mpango wa Marekani washtua***Inatoka Uk. 11*

kutoka Zambia na mashariki mwa DRC, huku nchi hizo zikipata unafuu wa kufirisha bidhaa kupitia Lobito zinaweza kuitumia bandari hiyo kusafirisha mizigo yao mingi kuelekea nje.

Jambo hilo linaweza kuwa pigo kubwa wa bandari ya Dar es salaam ambayo inaiangalia Zambia na DRC kama sehemu ya wateja wake wakubwa.

Hata hivyo, lengo la Marekani ni kuhakikisha kuwa Tanzania inahusishwa katika mpango huo ili kuunganisha usafiri wa shehena kupitia Bahari ya Atlantiki na Bahari ya Hindi ili kuirahisishia nchi hiyo usafirishaji wake wa shehena kuelekea Asia na Mashariki ya Mbali.

“Kwa maana hiyo, kuna uwezekano kiasi hiki cha fedha kikatumika kuifungua Angola kupitia Lobito na hilo likifanyika, Zambia na DRC zitaanza kuitumia Bandari ya Lobito kwa sababu watafupisha sana umbali ukilinganisha na Bandari ya Dar es Salaam,” alisema.

Marekani yajiingiza

Reli hiyo ya Benguela, ambayo ni kiungo muhimu cha usafirishaji nchini Angola, ilijengwa na China kwa lengo la kujihakikishia uhakika wa usafiri wa rasilimali zinazopatikana katika ukanda huo.

Kwa miaka kadhaa kumekuwa na jitihada za kuifufua reli hiyo.

Kwa sehemu kubwa jitihada hizo zilihusisha kampuni kutoka China, lakini hivi sasa Marekani nayo imeonekana kutia mguu katika mradi huo.

Fedha hizo kiasi cha dola milioni 250 ambazo zimetangazwa kutolewa hivi karibuni ni sehemu ya jitihada za Rais wa Marekani, Joe Biden, “kuimarisha uhusiano” na nchi zinazendelea kupitia uwekezaji.

Alitoa ahadi hiyo hivi karibuni katika kikao cha nchi saba tajiri duniani yaani G-7.

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa na uchumi wanaamini kuwa hii ni moja ya

*Rais wa Marekani Joe Biden*

mikakati ambayo Marekani imejiwekea kupambana na China katika kupanua nafasi yake katika biashara barani Afrika.

Aidha, Marekani inaiona reli hiyo kama kiungo muhimu na nafuu cha usafirishaji wa bidhaa zake na masuala ya usalama kwani reli hiyo itafupisha safari za kuzunguka Afrika Kusini au kupitia eneo la Mashariki ya Kati ambako “hakujatulika kiusalama.”

Ujenzi wa reli hiyo inayounganisha nchi ya Angola na Bandari ya Lobito nchini DRC ulianzishwa na wakoloni wa Ureno mwaka 1899 kwa lengo la kurahisisha usafiri kwenye eneo hilo lenye rasilimali nyingi.

Pamoja na Angola, lakini reli hiyo pia inapita katika maeneo yenye utajiri wa shaba nchini Zambia.

Kwa miaka kadhaa reli hiyo ilitumika kama njia kuu ya usafirishaji wa madini na rasilimali nyingine kutoka katika eneo hilo la kusini mwa Afrika kwenda Ulaya na Marekani.

Chalamila asimchulie Rais Samia

Na John MAGUHLA

KAULI ya wiki iliyopita ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila kwamba Rais Samia Suluhu Hassan – kwa “kununua ndege ya mizigo,” basi asitokee mtu yeyote kugombea kiti anachikalia sasa katika Uchaguzi Mkuu wa 2025.

Kwamba ujio wa ndege hiyo ndiyo kipimo cha kazi zilizotukuka za Rais Samia tangu ahamie Ikulu na kukalia kiti cha uongozi wa Tanzania pale ofisini kwake Magogoni, Dar es Salaam na kule Chamwino, Dodoma.

Chalamila anasema kwamba ili kuendelea kuimarisha kampeni hiyo, anatarajia kuanza na vikao vingi na viongozi wa karibu zaidi na wananchi, akianza na viongozi wa dini; wakuu wa madhehebu ili kufikisha ujumbe wake.

Lengo lake Chalamila ni kuwatumia viongozi hao wa imani kuwaeleza waumini wao kwamba Rais Samia “anatosha” na ahitaji kuwepo mtu mwingine kugombea nafasi ya urais.

Nia ya Chalamila kuwatumia viongozi wa dini ni sawa na kutangaza kwamba yeyote mwingine atakayenyanyuka kuchuana na kuomba ridhaa kutoka kwa wananchi dhidi ya Rais Samia, atakuwa “anachuma dhambi.”

Chalamila endapo kweli amedhamiria kumpigia debe la “kupita bila kupingwa” bosi wake, basi anaungana na watu wengine wanaojiita chawa, bila kujua kwamba wanamharibia sana Rais Samia katika “kuvuta mashabiki wake.”

Inaeleweka kuwa Chalamila – kwa kuamua kufanya hivyo, pamoja na mengine, anapigania ugali wake kwani Rais Samia ndiye mwajiri wake, hata kama mshahara analipwa na wananchi walipakodi wa Tanzania.

Uchawa huu wa Chalamila, unaweza kuwa hatari mno kwa ustawi wa demokrasia na unabeba dalili mbaya huko tuendako, kwamba mkuu huyo wa mkoa, anaweza kufanya lolote linalowezekana



Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila

ili kuhakikisha Rais Samia anabaki peke yake kwenye kinyang’anyiro cha kuwania uongozi wa juu wa Tanzania.

Ni vyema na haki sasa, endapo alichosema Chalamila, siyo utani, aanze kukemewa na ninaomba viongozi wa dini wakatae kupokea hoja ya Chalamila endapo atawaita na kulazimisha wasambaze “uchawa” ambao haufai katika Tanzania ya sasa.

Kwa namna anavyoendelea kufanya kazi zake, Rais Samia ameteka mioyo ya watu wengi, hata wale waliokuwa wakionekana kumpinga kwa baadhi ya mambo, wamemuelewa na sasa ni wafuasi wake kindakindaki.

Haki ya kupiga kura na hata raha ya uchaguzi ni kuwepo kwa ushindani na matokeo kutangazwa, sasa Chalamila anaposema viongozi wa dini washiriki kusambaza ujumbe kwamba kushindana na Rais Samia ni dhambi, anataka nini?

Je, Chalamila amenusa nini? Woga wake unatoka wapi? Ama kweli chawa ni mzigo kwa nchi yetu. Wakemewe!

Mbona Rais Samia mwenyewe hana wasiwasi na uchaguzi ujao, ndiyo maana anaendelea na kazi zake, sasa kiherehere cha Chalamila kinatoka wapi?

Habari Picha

UMEME



Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan akiwa na mwenyeji wake, Rais wa Uganda, Yoweri Kagame Museveni katika usinduzi wa Mradi wa Kufua Umeme wa Kikagati-Murongo, Wilaya ya Isingiro, huko Uganda.

Mradi huo wa umeme baada ya kusinduliwa utanufaisha pia wananchi wa Tanzania hasa wa maeneo ya wilaya za Kyerwa na Karagwe, Kagera kwa umeme wa gharama nafuu.

Shughuli ya usinduzi wa mradi huo zilifanyika Mei 25. (Picha na Ikutu).



Tangaza na Pambazuko

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.



Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au Barua-
Pepe; info@pambazuko.tz

Makala**Kiini cha mgogoro wa Sudan**

Na Mwandishi MAALUM

MWAKA jana, 2022 - Mwenyekiti wa Baraza la Kijeshi la Sudan, Jenerali Abdel Fattah al-Burhan alifanya mabadiliko ya kushitukiza ya uongozi wa Idara ya Usalama wa Taifa ya Sudan (GIS).

Mabadiliko haya ndiyo yamezaa na kuwa chimbuko la kuwepo kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe ambavyo vimesababisha vifo, uharibifu wa mali na miundombinu.

Ni kutokana na mabadiliko hayo, hivi sasa Sudan haitawaliki. Imegeuka kuwa uwanja wa mapambano na umwagaji damu ambao hata jumuiya za kimataifa zinaonekana kushindwa kuleta amani.

Mabadiliko hayo ya uongozi ndani ya idara nyeti ya usalama wa taifa ambayo kipindi cha utawala wa Rais Omar al-Bashir kabla ya kupinduliwa 2019, GIS, ilikuwa ikijulikana kwa jina maarufu la "Al Watani" (Jihaaz Al Amn Wal Mukhaabaraat Al Watani) ikiongozwa na moja ya mashushushu mahiri, Salah Gosh, ndiyo hasa kiini cha vita hivyo.

Jeshi lilipochukua nchi baada ya kumpindua Omar al-Bashir, kwa haraka wakafanya mabadiliko makubwa ya kimumo na uongozi wa idara hiyo.

Idara ikabadilishwa kutoka "Al Watani" na kuwa GIS (General Intelligence Services) halafu Salah Gosh akalazimishwa kujiuzulu na nafasi yake kuchukuliwa Jenerali Abu Bakr Mustafa akitokea jeshini.

Jenerali Mustafa ameiongoza GIS tangu kipindi hicho mpaka kufikia mwaka jana ambapo Mwenyekiti wa Baraza la Kijeshi Jenerali, Abdel al-Burhan alipomteua Ahmad Ibrahim Mufaddal kuwa mkuu mpya wa GIS.

Huyu Jenerali Mufaddal ambaye aliteuliwa kuwa kiongozi wa GIS anafahamika kuwa moja ya kinara wa kundi la watu ambao pale Sudan wanaitwa "Keizan".

Hawa "Keizan" ni watu wenye



Rais wa Sudan aliyepinduliwa Omar al-Bashir

msimamo mkali wa kidini na pia ni wafuasi wakubwa wa Omar al-Bashir.

Hawa Keizan wana uhasama mkubwa na Jenerali Hamdan Dagalo "Hemedti" ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Kijeshi linaloongoza nchi ya Sudan na pia ndiye mwanzilishi na kamanda mkuu wa vikosi vya RSF (Rapid Support Force).

Yaani kwamba, Mwenyekiti wa Baraza la Kijeshi, Jenerali al-Burhan alimteua mtu ambaye ni hasimu wa makamu wake kuongoza idara nyeti ya usalama wa taifa.

Sasa, kwa nini Jenerali Dagalo, Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Kijeshi linaloongoza Sudan na Kamanda Mkuu wa RSF ana uhasama mkubwa na mkurugenzi mpya wa GIS pamoja na watu wa kundi la 'Keizan'?

Ili kuelewa uhasama wao huu na namna gani umekuja kuchochea kuibuka kwa haya mapigano ambavyo yanaendelea, inapaswa kwanza kuelewa RSF na chimbuko lake.

Mara nyingi watu wakijadili mgogoro wa Sudan wanataja RSF kuwa ni vikosi vya "waasi" na pia RSF siyo sehemu ya jeshi la nchi.

Ni vikosi vya kijeshi ambavyo viko kihalali kisheria hapo Sudan lakini siyo sehemu ya vikosi vya jeshi la nchi.

Kiini cha mgogoro wa Sudan

Inatoka Uk. 16

Namna gani?

Miaka ya zamani kidogo, mwanzoni mwa 2000s Sudan ilikuwa na machafuko ya vita vya wenyewe kwa wenyewe kwenye maeneo ya magharibi na kusini mwa nchi hiyo.

Vita hivi vilikuwa vinasababishwa na makabila tofauti kugombea maeneo ya ardhi kwa ajili ya malisho ya mifugo na kilimo.

Maelfu ya watu walipoteza maisha katika vita hivyo.

Makabila ya maeneo ya magharibi wakaunda vikundi vyenye silaha kwa ajili ya kutetea jamii zao. Vikundi hivi vinajulikana jina maarufu la Janjaweed.

Baadaye hivi vikundi vya Janjaweed viliungana na kuunda chombo kimoja kilichoitwa “Quwwat ad-da[m] as-sari” na kiongozi wao akiwa ni Hamdan Dagalo maarufu kwa jina la “Hemedti”.

Kadiri miaka ilivyosonga, vikundi hivi vilizidi kulimbikiza ushawishi na nguvu kubwa ya kijeshi.

Sasa, mwaka 2009 Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu wa Kivita (ICC), walipotoa hati ya mashtaka dhidi ya al-Bashir, ilisababisha upepo wa kisiasa kubadilika sana Sudan.

Kulienea minong’ono, kwamba

majenerali kadhaa jeshini na hata Mkurugenzi ya Usalama wa Taifa wa kipindi hicho, Salah Gosh walikuwa wanataka Omar al-Bashir atolewe madarakani kwa maslahi mapana ya nchi ili kuepuka nchi kuwekewa vikwazo vya kimataifa na kutengwa na jamii ya kimataifa.

Minong’ono hiyo ilikuwa mikubwa kiasi kwamba ikamfanya Omar al-Bashir kuchukua hatua kadhaa za kujilinda ili asipinduliwe.

Kwanza alimfukuza kazi Salah Gosh kutoka kwenye nafasi ya ukurugenzi wa idara nyeti ya usalama, ingawa baadae akafanya makosa ya kumrejsha tena kwenye nafasi hiyo mwaka 2018.

Wakati anamrudisha, al-Bashir, akatumia mbinu za madikteta wengi kuruhusu uwepo na kushamiri kwa vikosi vya kijeshi mbadala nje ya jeshi la nchi ambavyo vitakuwa na uwezo kulidhibiti jeshi rasmi kama likitaka kufanya mapinduzi.

Katika kutekeleza mpango huu dhidi ya jeshi lake la nchi, al-Bashir akafanya makubaliano na Hamdan Dagalo, kiongozi wa vile vikundi vya Janjaweed, na kupitia hayo makubaliano yao ndio ikaundwa vikosi vya Rapid Support Force

Endelea Uk. 18



Mapigano ya wenyewe kwa wenyewe

Makala

Kiini cha mgogoro wa Sudan

Inatoka Uk. 17

(RSF).

Yaani kwamba, vile vikundi vya Janjaweed vilivyoungana, vikatambuliwa kisheria na kupewa jina jipya la RSF. Kamanda mkuu wa vikosi hivi vipya akiwa ni Hamdan Dagalo.

Huu ulikuwa ni mpango wa al-Bashir kujaribu kulidhibiti jeshi lake ili lisiweze kumpindua, na kwa hivyo ili vikosi hivi vipya vya RSF viwe na uwezo wa kudhibiti jeshi la nchi havipaswi kuwa chini ya jeshi la nchi, wala havipaswi kuwa tawi au vikosi maalumu vya jeshi rasmi la nchi.

Vinapaswa kuwa vikosi vinavyojitegemea moja kwa moja bila kuwa na uwezekano wa kupokea amri kutoka jeshi la nchi.

Ili kuifanya RSF isihusiane na jeshi la nchi, al-Bashir akaiweka RSF chini ya Idara ya Usalama wa Taifa - "Al Watani".

Kwamba, kisheria RSF ikatambulika kama vikosi vya kijeshi vya Idara ya Usalama wa Taifa.

Kwa miaka yote ambayo al-Bashir alikuwa Rais, RSF ilijitana sana na kuwa na nguvu kubwa mno kiasi kwamba al-

Bashir akawapa wao RSF jukumu la kumlinda yeye rais, kulinda ikulu na taasisi nyeti za nchi.

Lakini, mwaka 2019 RSF wakafanya kitu ambacho hakikutegemewa. Wakakubaliana na jeshi la nchi na kuruhusu jeshi lipindue serikali ya al-Bashir.

RSF wao ndio ambao walimkamata Rais al-Bashir kutoka Ikulu siku ya mapinduzi.

Kitendo hiki cha RSF kuruhusu al-Bashir apinduliwe, kimefanya mpaka leo hii watu wa 'Keizan' kuwaona RSF kama wasaliti na hivyo kuzaa uhasama wa kiapo baina yao.

Sasa, kitendo cha mwaka jana Mwenyekiti wa Baraza la Kijeshi la Sudan, Jenerali Abdel Al-Burhan kumteua Jenerali Ahmad Mufaddal kuwa mkurugenzi mpya wa Idara ya Usalama wa Taifa, huku ikijulikana wazi kwamba Mufaddal ni mtu wa 'Keizan' mfuasi kindakindaki wa Omar al-Bashir. ni dhahiri mpasuko mkubwa ungetokea.

Swali la msingi la kujjuliza, ni kwa nini Jenerali al-Burhan afanye uteuzi wa chokochoke ya wazi ya namna hii?



Maandamano yasiyoisha Sudan



Baadhi ya mashabiki na wapenzi wa Timu ya Yanga waliosafiri pamoja na timu hiyo kutoka Dar es Salaam, Tanzania kwenda Algiers, Algeria, wakionekana katika picha mbalimbali ndani na nje ya Uwanja wa July 5. Yanga ilisafiri kwenda huko kumaliza mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika ambapo ilicheza dhidi ya USM Alger ya Algeria. Yanga ilishinda 1-0, ingawa haikuwa bingwa wa Afrika baada ya kanuni za magoli ya ugenini. Yanga ilifungwa 2-1 na timu hiyo Dar es Salaam katika mchezo wao wa kwanza. (Picha na mitandao).

NI MAYELEEE...



Mshambuliaji wa Timu ya Yanga, Fiston Kalala Mayele amezawadiwa tuzo ya mfungaji bora wa michuano ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF) katika msimu wa 2022/23 baada ya kuibuka kinara wa kupachika magoli katika mashindano hayo yaliyofika tamati Jumamosi - Juni 3, jijini Algeria, Algeria. Alifikisha magoli saba. (Picha na Mtandao).

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

